**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**ILIYOKAA DAR ES SALAAM**

**MAREJEO NAMBA 606 YA 2019**

**BAINA YA**

**MAJUTO SHISHWA..............................................MLETA MAOMBI NA. 1**

**PHILIMON MJANJA ZOLA.....................................MLETA MAOMBI NA. 2**

**ALLY MOHAMED MAKUWA....................................MLETA MAOMBI NA. 3**

**NA**

**ESTIM CONSTRUCTION..............................................MJIBU MAOMBI**

Labour Court Tz

## HUKUMU

Tarehe ya Amri ya Mwisho: 15/04/2021

Tarehe ya Hukumu: 11/06/2021

**A. E. MWIPOPO, J**

Majuto Shishwa, Philimon Mjanja Mzola na Ally Mohamed Makuwa ambao ni Waleta Maombi katika shauri hili wameleta maombi haya ya marejeo kupinga uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika Mgogoro Na. CMA/DSM/KIN/R.1011/18/278 uliotolewa tarehe 31 Mei, 2019 na Mhe. P. Nyagaya, Muamuzi. Waleta Maombi wanaiomba Mhakama iitishe, ifanyie marejeo na kuweka pembeni tuzo iliyotolea na Tume katika mgogoro huo. Maombi haya yameambatishwa na Kiapo cha Majuto Shishwa ambaye ni Mleta Maombi Na. 1. Kiapo hicho kina hoja mbili za kisheria za marejeo katika aya ya 4 ya kiapo zinazotokana na ushahidi. Hoja hizo ni kama zifuatazo;

i. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi haikuuchambua ushahidi vizuri.

ii. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilikosea kusema Waleta Maombi hawakuwa wameajiriwa na Mjibu Maombi.

Historia ya mgogoro huu kwa ufupi ni kuwa Waleta Maombi wanadai kuwa waliajiriwa na Mjibu Maombi kwa mkataba wa maneno kama walinzi. Majuto Shishwa anadai aliajiriwa tarehe 17 Mei, 2016, Philemon Mjanja Mzola anadai aliajiriwa tarehe 20 Januari, 2015 na Ally Mohamed anadai aliajiriwa tarehe 24 February, 2013. Na mnamo tarehe 28 Septemba, 2018 waliachishwa kazi na kulipwa shilingi 400,500/= kila mmoja na kuambiwa kuwa mikataba yao imefika mwisho. Waleta Maombi hawakuridhika na uamuzi wa Mjibu Maombi ndipo wakafungua mgogoro wa kazi mbele ya Tume. Tume ilitoa uamuzi wake tarehe 31 Mei, 2019 na kuona kuwa hakukuwa na mahusiano ya kiajira baina ya pande hizo mbili. Waleta Maombi hawakuridhika na uamuzi huo wa Tume ndipo wamefungua shauri hili la marejeo Mahakamani.

Maombi haya ya marejeo yalisikilizwa kwa njia ya maandishi kufuatia amri ya Mahakama. Na pande zote ziliweza kuwaleta mawasilisho yao kwa wakati.

Akiwasilisha kuunga mkono marejeo haya, Bw. Nickson Ludovick, ambaye ni wakili anayewawakilisha Waleta Maombi alieleza kuwa Muamuzi alikosea kisheria na kiushahidi kuamua kuwa Waleta Maombi hawakuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi kwa sababu Waleta Maombi hawakuwa na mkataba wa ajira na Mjibu Maombi. Kwa mujibu wa kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi za Kazi,

Labour Court Tz

2004, waajiriwa hawahitaji mkataba wa maandishi ili kuwa wameajiriwa. Kinachotakiwa ni kuonesha kuwa mwajiriwa alikuwa akifanya kazi kwa mwajiri na ni mwajiri ndiye aliyekuwa akimlipa na kumpa amri na kazi za kufanya. Waleta Maombi walitoa ushahidi wa karatasi za kupokea mizigo (delivery note) – kielelezo A1, karatasi ya mahudhurio – kielelezo A2 na barua ya onyo – kielelezo A3 na karatasi ya kupangiwa kazi ambapo vielelezo hivyo pamoja na ushahidi wa Majuto Shishwa kwa pamoja ulithibitisha kuwa Waleta Maombi walikuwa ni waajiriwa wa Mjibu Maombi.

Wakili alieleza kuwa hoja ya Muamuzi kuwa Waleta Maombi waliajiriwa na kampuni ya ulinzi ambayo ndio iliyokuwa imepewa kazi na Mjibu Maombi ni dhaifu kwa sababu hakuna mkataba baina ya Mjibu Maombi na kampuni hiyo. Pia hakukuwa na ushahidi wa uliotolewa. Pia hakuna mtu yoyote kutoka katika hiyo kampuni ambayo inadaiwa kupewa kazi aliyetoa ushahidi na hakuna sababu iliyotolewa ni kwanini shahidi huyo ambaye ni wa msingi hajaitwa kutoa ushahidi. Kwa kuwa Mjibu Maombi alitoa maelezo hayo alikuwa na wajibu wa kuyathibitisha kwa mujibu wa kifungu cha 110(1) na 111 cha Sheria ya Ushahidi ya Tanzania, Sura ya 6 ya Sheria, Kama Ilivyorejewa mwaka 2002.

Wakili aliendelea kueleza kuwa Muamuzi alikosea kuona kuwa Mjibu Maombi aliwasilisha kama vielelezo nyaraka ambazo ni orodha ya malipo ya wafanyakazi (payroll), orodha ya WCF, Orodha ya PPF na orodha ya watumishi

wa Mjibu Maombi ambapo katika nyaraka hizo majina ya Waleta Maombi hayapo. Hoja hii ni dhaifu kwanini haitegemewi kwa Mjibu Maombi hatarajiwi kuleta ushahidi ulio kinyume na Shauri Lake. Nyaraka hizo ziliandaliwa na Mjibu Maombi hivyo kuna uwezekano wa Mjibu Maombi kuondoa Majina ya Waleta Maombi na Muamuzi alitakiwa kuliona jambo hilo.

Wakili wa Waleta Maombi alimalizia kwa kueleza kuwa uamuzi alikosea kisheria na kiushahidi kuona kuwa Waleta Maombi hawastahili nafuu yoyote. Waleta Maombi waliomba likizo ambazo hazijalipwa, malipo ya saa za kazi za ziada ambayo hayajalipwa kwa kuwa walikuwa wanafanya kazi kwa masaa 12 na mafao mengine ambayo yapo katika fomu Na. 1 ya Tume. Pia kuna mapunjo ya mishahara yao ambayo walikuwa wakilipwa shilingi 8,000/= badala ya shilingi 12,000/= kwa siku ambayo ni tofauti ya shilingi 4,000/=. Hivyo, Waleta Maombi wanaomba wapatiwe nafuu walizoziomba na marejeo haya yakubaliwe. Na uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na uamuazi ufutwe.

Akijibu mawasilisho ya Waleta Maombi, Wakili anayemwakilisha Mjibu Maombi aitwaye Musa Mbaga alieleza kuwa Tume ilikuwa sahihi kuona kuwa hakukuwa na uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa baina ya Waleta Maombi na Mjibu Maombi na kwa sababu hiyo hawastahili nafuu yoyote. Kwa sababu hiyo wanakanusha na kupinga hoja za Waleta Maombi na mawasilisho yao. Waleta Maombi waliajiriwa na Kampuni ya ulinzi ambayo ndio ilikuwa inatoa huduma ya ulinzi kwa Mjibu Maombi katika majengo yake tofauti tofauti hivyo Mjibu



Labour Court TZ

Maombi hajawahi kuwaajiri. Waleta Maombi walishindwa kuleta uthibitisho wowote kuwa walikuwa wameajiriwa na Mjibu Maombi. Hata namna ambayo Waleta Maombi walikuwa wakifanya kazi inaonesha kuwa hawakuwa chini ya usimamizi na maelekezo ya Mjibu Maombi bali walikuwa chini ya kampuni ya ulinzi. Kifungu cha 4 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004, kinatoa tafsiri ya mwajiriwa kuwa ni mtu ambaye ameingia mkataba wa ajira au ameingia mkataba mwingine wowote kwa ajili ya kufanya kazi yeye mwenyewe kwa upande mwingine wa makataba na huo upande mwingine sio mteja wa ujuzi wa aina yoyote, biashara au shughuli inayofanywa na mtu binafsi; au mwajiriwa ambaye ametambuliwa na Waziri chini ya kifungu 98(3).

Wakili wa Mjibu Maombi alieleza kuwa ni wazi kuwa ushahidi uliotolewa mbele ya Tume unaonesha kuwa hakukuwa na mkataba wa aina yoyote ile. Na kuwa kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi za Kazi hakiwahusu Waleta Maombi kwa kuwa ukiangalia mazingira ya kazi, sheria hiyo haiendani na mazingira haya. Waleta Maombi hawakuwa chini ya usimamizi wa Mjibu Maombi katika namna ya kufanya kazi zao, masaa yao ya kazi, hawakuwa ni sehemu ya muundo wa mjibu maombi kama taasisi, ni kampuni ya ulinzi ambayo ndio ilikuwa ikitoa huduma kwake, Waleta Maombi hawajawahi kumtegemea kiuchumi na hakuwa akiwapatia vitendea kazi. Kwa sababu hiyo, vigezo vyote vilivyowekwa na kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi za Kazi ni wazi kuwa hakukuwa na mahusiano ya mwajiri na mwajiriwa. Kuunga Mkono hoja yake

Wakili alinukuu kesi ya **TIFPA** dhidi ya **Aloyce Byaro**, Marejeo Na. 02 ya 2019, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, Iliyokaa Musoma; na kesi ya **Ismail Musa Athumani** dhidi ya **Lake Oil Ltd**, Marejeo Na. 86 ya 2019, Marejeo Na. 86 ya 2019, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, Iliyokaa Dar Es Salaam.

Aliendelea kueleza kuwa kielelezo A1, A2 na A3 zimeshindwa kuthibitisha mahusiano ya mwajiri na mwajiriwa baina yao. Vielelezo hivyo havithibitishi usimamizi wa Mjibu Maombi na pia havioneshi kuwa alikuwa akiwalipa mishahara. Karatasi ya mahudhurio imewekwa na kampuni ya ulinzi ikiwa ni namna ya kuwasimamia waajiriwa wao.

Kuhusu hoja kuwa Muamuzi alihamisha wajibu wa kuthibitisha (burden of proof), Mjibu alieleza kuwa mgogoro uliopo ni kuhusu uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa na sio mgogoro wa uachishwaji kazi ambao ndio wajibu wa kuthibitisha uachishwaji kazi ni wa mwajiri. Pia kuhusu hoja kuwa Mjibu Maombi kurekebisha orodha ya PPF na WCF kwa kuondoa majina ya Waleta Maombi, jibu Maombi alieleza kuwa hoja hiyo sio sahihi na kuwa nyraka hizo ni za taasisi za Serikali na zinaonesha kuwa Waleta Maombi hawajawahi kuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi. Kwa sababu hiyo, Waleta Maombi hawastahili nafuu wanazoziamba na Mjibu Maombi anaomba Marejeo haya yatupiliwe mbali (dismissed) na uamuzi wa Tume uendelee.

Waleta Maombi hawakuwasilisha mawasilisho yao ya nyongeza (rejoinder submission).



Labour Court TZ

Baada ya kuangalia kwa muhtasari mawasilisho ya pande zote mbili, Mahakama ipo katika nafasi ya kuangalia hoja zilizowasilishwa na pande zote mbili.

Nikianza na hoja ya Waleta Maombi kuwa Muamuzi alikosea kisheria na kiushahidi kuamua kuwa Waleta Maombi hawakuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi kwa sababu Waleta Maombi hawakuwa na mkataba wa ajira na Mjibu Maombi, Waleta Maombi walieleza kuwa ushahidi wa karatasi za kupokea mizigo (delivery note) – kielelezo A1, karatasi ya mahudhurio – kielelezo A2 na barua ya onyo – kielelezo A3 ambapo vielelezo hivyo pamoja na ushahidi wa Majuto Shishwa kwa pamoja ulithibitisha kuwa Waleta Maombi walikuwa ni waajiriwa wa Mjibu Maombi hata bila ya kuwa na mkataba wa maandishi. Kwa upande mwingine, Mjibu Maombi alieleza kuwa ushahidi uliotolewa na Waleta Maombi ulishindwa kuthibitishwa kuwa walikuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi.

Kifungu cha 61 cha Sheria ya Taasisi cha kazi ndicho kinachoeleza mazingira ambayo mwajiriwa ambaye hana mkataba wa kazi anadhaniwa kuwa ni mwajiriwa. Na mazingira hayo ni namna mtu huyo anavyofanya kazi chini ya usimamizi au maelekezo ya mtu mwingine, masaa anayofanyia kazi kuwa chini ya usimamizi au maelekezo ya huyo mtu mwingine, kuwa sehemu ya mfumo iwapo anafanyia kazi katika taasisi, kufanya kazi kwa zaidi ya saa 45 kwa mwezi kwa miezi 3 mfululizo, kumtegemea mtu anayemfanyia kazi kiuchumi, kupewa vifaa vya kazi na kufanya kazi kwa huyo mtu mmoja tu. Na kwa kuwa mgogoro



LabourCourt TZ

huu hauhusu uhalali wa kuachishwa kazi, ni wajibu wa Waleta Maombi ambao wanadai kuwa walikuwa ni waajiriwa wa Mjibu Maombi kuthibitisha hivyo. Na hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 110(1) na 111 cha Sheria ya Ushahidi ya Tanzania, Sura ya 6 ya Sheria (Tanzania Evidence Act, Cap. 6 of the Laws).

Katika kesi ya **Mwita Wambura** dhidi ya **Zuri Haji, Marejeo Na. 42 ya 2012, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyokaa Mwanza,** Mahakama ilikuwa na maoni kuwa kuna mambo ya kawaida ambayo yanaweza kumsaidia mtu anayefanya uamuzi kuamua kuhusu uwepo wa mahusiano ya ajira. Mambo hayo ni majukumu ya pande zote ikiwa ni pamoja na utegemezi, maelekezo, usimamizi, udhibiti na utii wa namna kazi ilivyokuwa inafanywa.

Ushahidi uliomo katika rekodi unaonesha kuwa shahidi pekee wa Waleta Maombi ambaye ni Majuto Shishwa alieleza kuwa waliajiriwa kwa mdomo na waliachishwa kazi baada ya kufungua mgogoro wa kudai mazingira na maslahi bora ya kazi mbele ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Na kuthibitisha kuwa walikuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi alitoa Mahudhurio ya Philemon Mzola – Kielelezo A1, Onyo la Maandishi alilopewa Philemon Mzola – Kielelezo A2, Mahudhurio ya Ally Mohamed – Kielelezo A3 na karatasi ya kupangiwa kazi – kielelezo A4. Kwa upande wa Mjibu Maombi alikuwa na mashahidi wawili ambao wote walisema kuwa Waleta Maombi hawakuwa waajiriwa wa Mleta Maombi. Kuthibitisha maelezo yao walitoa orodha ya michango ya PPF ya wafanyakazi

wa Mjibu Maombi wanaolipwa kwa siku – Kielelezo D1 na Orodha ya Michango ya WCF ya wafanyakazi wa Mjibu Maombi wanaolipwa kwa siku- Kielelezo D2.

Kutokana na ushahidi wa pande zote mbili ni wazi kuwa Waleta Maombi walikuwa na wajibu wa kuthibitisha madai yao ya kuwa walikuwa wameajiriwa na Mjibu Maombi. Ushahidi pekee walioutegemea ni Mahudhurio ya Waleta Maombi Na. 2 na Na. 3, Barua ya Onyo ya Mleta Maombi Na. 2, karatasi ya kufanyiwa kazi na karatasi ya kupokea mzigo ya kampuni ya Estim. Ushahidi huo ulipingwa na mashahidi wa Mjibu Maombi walioeleza kuwa mahudhurio hayo hayathibitishi kuwa walikuwa waajiriwa, na pia barua ya onyo haikuwa imeandikwa na Mjibu Maombi. Ni maoni yangu kuwa ushahidi huo wa Waleta Maombi unaonesha kuwa walikuwa wanafanyia kazi katika eneo la Mjibu Maombi lakini haliwezi kuthibitisha kuwa walikuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi. Na sababu ni kuwa kuna ushahidi mwingine ambao unapingana na maelezo yao na unaonesha kuwa Waleta Maombi hawakuwa wafanyakazi wao. Mambo yanayoweza kuthibitisha mahusiano ya ajira baina ya Waleta Maombi na Wajibu Maombi ni ushahidi kuwa walikuwa wakipatiwa kazi chini ya utegemezi, maelekezo, usimamizi na udhibiti wa Mjibu Maombi na kuwa walikuwa wanatiii maelekezo yake. Aidha, kuna kielelezo A4 ambayo ni karatasi inayoonesha Waleta Maombi wakipangiwa kazi kazi jengo la Vijana na Vijana II ambayo haijaelezwa iwapo ni maeneo ya Mjibu Maombi.

Nimeangalia uamuzi wa Tume ambapo Muamuzi aliona kuwa Waleta Maombi walishindwa kuthibitisha kuwa Mjibu Maombi ndie aliyekuwa akilipa mishahara yao, aliwasimamia na kuwaelekeza kazi. Nakubaliana na uamuzi huo wa Tume kwa kuwa katika ushahidi wao mbele ya Tume Mleta Maombi Na. 1 hajaeleza iwapo walikuwa wakilipwa mishahara na Mjibu Maombi. Alichoongelea ni kulipwa posho ya shilingi 5,000/= kwa siku ya kushika silaha ya moto. Hivyo, hakuna ushahidi unaoonesha kuwa Mjibu Maombi alikuwa amewaajiri Waleta Maombi na kuwa kulikuwa na mahusiano ya mwajiri na mwajiriwa baina yao. Kwa sababu hiyo, naona kuwa ushahidi uliopo hautoshi kuthibitisha kuwa Waleta Maombi walikuwa wameajiriwa na Mjibu Maombi.

Kuhusu hoja ya Waleta Maombi kuwa Muamuzi alikosea kisheria na kiushahidi kuona kuwa Waleta Maombi hawastahili nafuu yoyote. Kwa kuwa nimeona kuwa Waleta Maombi hawakuwa wameajiriwa na Mjibu Maombi ni wazi kuwa hawastahili nafuu yoyote ya likizo, malipo ya saa za kazi za ziada na mafao mengine ya kuachishwa kazi. Aidha, kuhusu mapunjo ya mishahara yao hakuna ushahidi kuwa walikuwa wanalipwa na Mjibu Maombi au kuwa kuna malipo walikuwa wanapunjwa. Aidha, kwa kuwa nimeona kuwa Waleta Maombi hawakuwa waajiriwa wa Mjibu Maombi hawastahili kulipwa malipo yoyote ya mapunjo ya mishahara kwa kuwa Mjibu Maombi hakuwa mwajiri wao. Hivyo, nakubaliana na Tume kuwa Waleta Maombi hawastahili kupata nafuu yoyot kati ya walizoomba.

Kwa sababu hiyo, shauri hili nalitupili mbali (dismissed) kwa kuwa halina mashiko. Uamuzi wa Tume unaendelea kuwa kama ulivyotolewa. Kila upande utajigharamia gharama zake za kuendesha shauri hili.

**A. E. MWIPOPO**
**JAJI**
**11/06/2021**

Labour Court Tz